WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA AWALI NA MAFUNZO YA UFUNDI
KAZI YA RIKIZO MEI 2020
KISWAHILI VI

JINA: _____ TAREHE: _____

SEHEMU A: SARUFI

1. Msichana mrembo anakimbia.kivumishi katika sentensi hii ni kipi?_____
   (a) Msichana (c) Anakimbia
   (b) Mrembo (d) Hakuna

2. Musa alihukumiwa kunyongwa. Sentensi hii ipo katika hali ipi ya vitenzi_____
   (a) Hali isiyoridhika (c) Hali ya kutendeka
   (b) Hali iliyopo (d) Hali timilifu

3. Amina ni kitoto kitundu sana. Neno qani limetumika kama kitenzi kishirikishi _____
   (a) Amina (c) Kitundu
   (b) Ni (d) Sana

4. Mzizi wa neno katika neno walikula ni _____
   (a) Wali (c) Kula
   (b) Kali (d) Lik

5. Timu ya mpira ingalicheza mchezo huu ingalisha hii ni aina gani ya sentensi_____
   (a) Changamano (c) Sahihi
   (b) Shurutia (d) Ambatano

6. Mwanafunzi amechapwa viboko. Sentensi hii ipo katika kauli ya_____
   (a) Katenda (c) Kutendewa
   (b) Kutendwa (d) Kutendeana

7. Alifika jana. Kiambishi kinachoonyesha wakati ni kipi?_____
   (a) A (c) Ja
   (b) Li (d) Ka

8. Neno lipi ni kinyume cha neno Ghasia?
   (a) Shwari (c) Ushirikiano
   (b) Upendo (d) Mshikamano

9. Nomino mkutano ipo katika aina ipi ya nomino?_____
   (a) Nomino ya kawaida (c) Za pekee
   (b) Za jumla (d) Dhahania

10. Tulimkuta rafiki yetu amelewa chakari. Neno chakari limetumika kama?_____
    (a) Nomino (c) Kiunganishi
    (b) Kielezi (d) Kitenzi

11. Angelijua maji ni marefu kiasi icho_____
    (a) Asingeliogelea
    (b) Asingaliogelea
    (c) Alingaliogelea
    (d) Angeogelea

12. Neno KWAMBA lina silabi_____
    (a) Mbili
    (b) Tatu
    (c) Tano
    (d) Sita

13. Neno ambalo halihusiani na mengine kati ya maneno yafuatayo_____
    (a) Mpera
    (b) Embe
    (c) Chungwa
    (d) Papai

14. Atakuja kesho. Silabi inayotambulisha wakati ujao ni _____
    (a) Ta
    (b) Sa
    (c) Li
    (d) Kuja

15. Alipoingia hakumkuta mtu _____
    (a) Yeyote
    (b) Ndani
    (c) Wowote
    (d) Silabi

SEHEMU B: MSAMIATI

16. Mtu asiye na pua huitwa _____
    (a) Shaibu
    (b) Toinyo
    (c) Nunge
    (d) Ajuza

17. Mtu msafi wa mavazi huitwa._____
    (a) Msafi
    (b) Nadhifu
    (c) Mtanashati
    (d) Mngavu

18. Jembe la kukokotwa na ng'ombe huitwa_____
    (a) Plau
    (b) Pilau
    (c) Masai
    (d) Jembe

19. Chukua kisu kisha _____ papai letu.
    (a) Tumbua
    (b) Menya
    (c) Toboa
    (d) Kata

20. Kisawe cha neno <u>karai</u> ni_____
    (a) Kauzu
    (b) Beseni
    (c) Ndovu
    (d) Pipi

21. Neno <u>katuzu</u> lina maana ya _____
    (a) Hakujia
    (b) Hakunufaika
    (c) Hitimu
    (d) Hakufaulu

22. Barua husafirishwa kwa njia ya _____
    (a) Posta
    (b) Stempu
    (c) Boksi
    (d) Upepo

23. Kipaji chake kili_____ alipokatazwa kukiendeleza.
    (a) Poa
    (b) Shida
    (c) Kua
    (d) Via

24. Kutokana na umaskini wake yule bibi yake alivaa nguo _____
    (a) Nyeupe
    (b) Nzuri
    (c) Kuu kuu
    (d) Fupi

25. Maana ya neno kumiliki ni _____
    (a) Kutawala
    (b) Kuhoji
    (c) Kuchana
    (d) Kutahadhari

SEHEMU C: METHALI, NAHAU NA VITENDAWILI

26. Methali isemayo "hamadi kibindoni" inafundisha nini?
    (a) Kutumia kile mtu alichonacho
    (b) Kutofuja mali kabla ya uzee
    (c) Kuweka faida ili itufae baadaye
    (d) Fuja mali kufa kwaja

27. Kamilisha sentensi ifuatayo "Mpofuka ukongweni"_____
    (a) Hapotei njia
    (b) Hakumbuka ujanani
    (c) Hakumbuki njia
    (d) Hukumbuka njia

28. Chembe na chembe mkate huwa. Methali nyingine yenye maana sawa na hii ni kipi?_____
    (a) Mwenda pole hajikwai
    (b) Haba na haba hujaza kibaba
    (c) Chovya chovyo humaliza buyu la asali
    (d) Ngoja ngoja yaumiza matumbo

29. "Jinamizi laniita lakini silioni" maana ya kitendawili hiki ni_____
    (a) Jua
    (b) Radi
    (c) Popo
    (d) Mwangwi

30. "Meno ya mbwa hayaumani" Methali ipi kati ya methali zifuatazo ina maana sawa na hii;-
    (a) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
    (b) Damu nzito kuliko maji
    (c) Asiyekutenda usimtende
    (d) Ukipenda chongo huita na kengeza

31. "Daima na msikia lakini simuoni" Maana ya kitendawili hiki ni kipi?_____
    (a) Upepo
    (b) Mchawi
    (c) Hewa
    (d) Shetani

32. Ipi ni maana sahihi ya usemi" Hatujui kwa heri wala kwa shari?_____
    (a) Hatusaidiani katika furaha wala huzuni
    (b) Hatujui wakati wa furaha
    (c) Salamu utolewa kwa kila mtu
    (d) Hatujali chochote

33. Maana ya nahau" Kupiga chuku ni ipi?_____
    (a) Kutoa maelezo ya uongo
    (b) Kusema ukweli daima
    (c) Kuchukia jambo Fulani
    (d) Kutia maneno chumvi

34. "Kila ukiwakuta wamejitayarisha kupigana" Kitendawili hiki kina maana ipi?_____
    (a) Askari
    (b) Katani
    (c) Wamasai
    (d) Nungunungu

35. Nahau isemayo "Anika juani" ina maana gani?_____
    (a) Sema kwa sauti
    (b) Toboa siri
    (c) Sema waziwazi
    (d) Sema na watu vizuri

SEHEMU D: UFAHAMU

Soma kifungu cha habari kisha ujibu maswali yafuatayo:

Ni jambo la ujinga kuchagua fedha na kuziweka awali kama chombo cha maendeleo. Ili hali twajua nchi yetu ni duni. Ni ujinga vilevile tukikazania hali hiyo ya unyonge kwa kutegemea fedha kutoka **ughaibuni** badala ya fedha zetu wenyewe. Ni ujinga kwa sababu mbili, kwanza hatuwezi kuzipata, ingawa zipo nchi yenye neema zinazoweza kutoa mikopo hiyo haitoshi kwa nchi changa kama Tanzania.

Kama twataka maendeleo hatuna budi kufanya kazi kwa bidii, juhudi na maarifa, misaada yaweza kuhatanisha usalama wa nchi.

MASWALI

36. Ili tuepuke na mikopo yatubidi _____
    (a) Tuombe misaada
    (b) Tuombe wataalam
    (c) Tusome sana
    (d) Tufanye kazi

37. Neno ughaibuni katika habari lina maana ya _____
    (a) Nchi tajiri
    (b) Nchi za kiarabu
    (c) Nchi maskini
    (d) Nchi za michache

38. Mwandishi anasem a _____
    (a) Fedha hhaiondoi unyonge
    (b) Tutegemee mikopo ya marafiki
    (c) Tutegemee mikopo michache
    (d) Fedhah ni msingi wa maendeleo

39. Neno duni kama lilivyotumika katika habari hii lina maana ya _____
    (a) Changa
    (b) Tajiri
    (c) Maskini
    (d) Maarufu

40. Kichwa cha habari hii chafaa kuitwa _____
    (a) Tuchague fedhah kwa maendeleo yetu
    (b) Fedhah ndio njia pekee ya kujiendeleza
    (c) Kujiendeleza huletwa na fedha
    (d) Fedha sio maendeleo ya nchi

Soma shairi hili kisha jibu maswali

1. Mama yangu simuoni, naambiwa kakimbia,
   Sina furaha moyoni, mama nilimzoea,
   Nimebaki ukiwani, ninalia na dunia,
   Kinda ningali mtini, sina mama kunilea.

2. Mama nilikosa nini, mwanao kunikimbia,
   Umenitupia nini, mwingine wa kunilea,
   Nimebaki na huzuni, sina wa kumdekea,
   Kinda ningali mtini, sina mama kunilea.

MASWALI

41. Shairi hili lina beti ----------
    (a) 16 (c) 4
    (b) 2 (d) 5

42. Vina vya kati vya ubeti wa kwanza na wa pili ni----------
    (a) Ni (c) A
    (b) Na (d) Wa

43. Neno umenitupia lina silabi ngapi? ----------
    (a) 4 (c) 8
    (b) 6 (d) 6

44. Mstari mmoja wa ubeti wa shairi huitwa----------
    (a) Mizani (c) Mizawa
    (b) Mshororo (d) Zania

45. Andika kwa neno moja majonzi, masikitiko, simanzi----------
    (a) Furaha (c) Hamaki
    (b) Huzuni (d) Hasira

SEHEMU E: UTUNGAJI
TAJA MAMBO MUHIMU (5) YALIYOKOSEKANA KWENYE BARUA HII!

SHULE YA MSINGI ULALI
(46)----------
MOSHI
(47) ----------

(48)----------
Dhumuni la barua hii ni kukujulisha kuwa nilipofika shuleni nilikuta ada imeongezeka. Ninaomba unitumie shilling elfu hamsini ili nimalize ada.

(49) ----------
(50)----------